JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

# MWONGOZO WA UPIMAJI WA WASAFIRISHAJI WANAOFANYA SAFARI ZA NJE YA NCHI

**Toleo la Kwanza Tarehe 20 Mei, 2020**

## 1.0 Utangulizi

Kutokana na wimbi kubwa la wasafirishaji wanaofanya safari kati ya Tanzania na nchi za Rwanda, Uganda, Kenya na Zambia kutolewa taarifa kuwa wamepata maambukizi ya ugonjwa wa COVID-19. Wizara imeandaa mwongozo kwa ajili ya kudhibiti maambukizi katika sekta ya Usafirishaji katika uchumi wa nchi. Kwa sasa wastani wa wasafirishaji 500 wanaingia nchini kupitia katika mipaka ya barabara kwa siku kati ya hao zaidi ya asilimia 50 ni watanzania na wengine ni kutoka katika nchi nyingine zikiongozwa na Burundi, Kenya, Uganda, Rwanda, Malawi na Zambia. Asilimia kubwa ya wasafirishaji hawa wanatokea Mkoa wa Dar es Salaam kuchukua mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam na Soko la Kariakoo.

### 1.1 Malengo ya Mwongozo

Mwongozo huu unalenga kuweka utaratibu na Mikakati ya Kukabiliana na Mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 kupitia Sekta ya Usafirishaji. Mwongozo huu unaweka utaratibu wa kupima wasafirishaji wa malori yanayobeba bidhaa muhimu na Mikakati ya Kukabiliana na Mlipuko na Ugonjwa wa COVID-19

## 2.0 Walengwa wa Mwongozo

Mwongozo huu unalenga watoa huduma za afya mipakani, wasafirishaji wa mizigo inayoingia na kutoka nchini, wamiliki wa vyombo vya usafiri, mamlaka za udhibiti wa usafirishaji kwa njia ya barabara, vyombo vya usalama na wengineo.

## 3.0 Kamati ya Usimamizi wa Upimaji na Udhibiti wa COVID-19 kwa wasafirishaji wa Malori.

### 3.1 Ngazi ya Taifa

**3.1.1 Wajumbe**: Afya Mipakani, Mwakilishi wa Mambo ya Nje, Maabara ya Taifa, Mwakilishi wa LATRA, Mwakilishi wa OR-TAMISEMI, Mamlaka ya Mapato

Tanzania, Mwakilishi wa Wizara ya Uchukuzi, Mwakilishi wa Usalama Barabarani na wawakilishi wa Vyama vya Wasafirishaji

**3.1.2 Majukumu**

1. Kuandaa Mwongozo wa udhibiti wa COVID-19 kupitia sekta ya usafirishaji.
2. Kuandaa utaratibu wa uchangiaji wa gharama za upimaji pale itakapohitajika.
3. Kuhakikisha kuna orodha ya wasafirishaji wote wanaofanya safari katika nchi mbalimbali na kutunza kanzi data yao.
4. Kupokea changamoto za zoezi la upimaji na kuzifanyia kazi
5. Kuhakikisha kuna vituo vya upimaji na vyenye vifaa vya kuchukulia sampuli
6. Kuhakikisha majibu ya upimaji yanatoka mapema
7. Kuhakikisha wanatoa vyeti kwa wale wasiokuwa na maambukizi ili kuendelea na usafirishaji
8. Kufanya usimamizi shirikishi na kuwajengea uwezo wapimaji.
9. Kuhakikisha wasafirishaji walioonekana kuwa na maambukizi wanapatiwa huduma za afya.
10. Kuratibu vikao vya wadau pamoja na vikao vya nchi jirani ili kuondoa changamoto za usafirishaji.

**3.2 Ngazi ya Mkoa na Mipakani**

**3.2.1 Wajumbe:** Mganga Mkuu wa Mkoa, Waganga wa kuu wa Wilaya ambapo Mipaka ipo, Maafisa afya wafawidhi wa Mipaka, Afisa uhamiaji, Afisa Usalama wa Barabarani wa Mkoa/Wilaya timu ya wachukua sampuli (daktari mmoja na nurse wawili) na Maafisa Usalama wa Taifa, Polisi na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Mganga Mkuu wa Mkoa atakuwa msimamizi wa zoezi hili.

**3.2.2 Majukumu**

1. Kuhakikisha vituo vya upimaji vimeainishwa na kuna watumishi wa kuchukua sampuli muda wote
2. Kuhakikisha uwepo wa vifaa muhimu vya kuchukulia sampuli kwa kuvichukua kutoka katika maabara ya taifa.
3. Kuhakikisha wasafirishaji wanapata majibu yao kwa wakati
4. Kupokea changamoto na kuzifanyia kazi
5. Kuhakikisha wasafirishaji ambao watakutwa na maambukizi wanafanyiwa *counselling* na kupewa njia sahihi za kuishi bila kueneza maambukizi kwa wengine
6. Kuhakikisha wanakutwa na maambukizi wanafuatiliwa na wanapata matibabu inapobidi
7. Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kuhakikisha wasafirishaji wana vyeti vya upimaji
8. Kuhakikisha wasafirishaji ambao wamepima POSITIVE hawaendelei na safari
9. Kukagua uzingatiaji wa matumizi ya vifaa kinga ikiwemo barakoa, sanitizer
10. Kuchukua sampuli kila siku na kuziwasilisha katika Maabara ya Taifa

11. Kuhakikisha kuna vituo vya upimaji na vyenye vifaa vya kuchukulia sampuli na utaratibu wa kufikisha sampuli maabara ya kupima
12. Kutoa kipaumbele cha sehemu ya kupaki gari Pamoja na ulinzi wa mizigo kwa kipindi chote cha kubadilisha wasafirishaji na kusubiri vipimo.

## 4.0 Utaratibu wa upimaji

### 4.1 Upimaji kabla ya Safari (Exit Screening)

4.1.2 Wasafirishaji hawataruhusiwa kusafirisha mizigo bila kufanyiwa vipimo na kuonekana hawana maambukizi ya COVID-19

4.1.3 Wamiliki wa vyombo vya usafiri kuhakikisha wasafirishaji wote wanaokwenda nje ya nchi wamepima na hawana maambukizi ya COVID-19.

4.1.4 Wasafirishaji watakuwa hawana maambukizi watapewa cheti maalumu ambacho kitaoneshwa mpakani (**Kiambatisho namba 01)**

4.1.5 Vipimo vya COVID-19 vitakuwa vinarudiwa kila baada ya siku 14 anapokuwa ametimiza incubation period bila kuonyesha dalili, hivyo atapimwa tena ili kufahamu hali yake.

4.1.6 Wamiliki wa vyombo vya usafiri wahakikishe wasafirishaji ambao wako Dar es Salaam wanakwenda kupima katika maabara ya Taifa iliyoko Mabibo External

4.1.7 Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa kwa kushirikiana na Mkuu wa Maabara yaTaifa watahakikisha kuna watumishi na vifaa muhimu kwa ajili ya zoezi la kuchukua sampuli kwa wasafirishaji na kuwapatia majibu kwa wakati.

4.1.8 Maafisa Afya wa Mipakani kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kukagua vyeti vya upimaji wa COVID-19. Ukaguzi huu uhusishe kulinganisha taarifa za dereva zilizoko katika kanzi data ya waliopima na cheti alichonacho.

4.1.9 Wasafirishaji ambao watakuwa wana cheti na hawapo katika kanzi data ya waliopima mpakani watachukuliwa kuwa hawajapima.

### 4.2 Upimaji wa Wasafirishaji ambao Safari hazitaanzia Mkoa wa Dar es Salaam.

4.2.1 Wasafirishaji ambao hawako Dar es Salaam watachukuliwa sampuli katika Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa baada ya kuonesha ushahidi wa safari za nje ya nchi (hati ya kusafiria au kitambulisho) au Mipakani na kusubiri majibu.

4.2.2 Sampuli zilizochukuliwa kwa wasafirishaji ziandikwe maneno ya utambulisho yaani ***Jina la Mpaka_TD***

4.2.3 Wamiliki wa magari ya usafirishaji wa mizigo wahakikishe wasafirishaji wao wamepima na kuwa na cheti kabla ya kuanza safari zao.

4.2.4 Msafirishaji ambaye ataonekana ana maambukizi ya COVID-19 hataruhusiwa kuendelea na safari hivyo lazima wamiliki walete dereva mwingine ambaye naye atapimwa.

4.2.5 Msafirishaji ambaye atabainika kuwa na maambukizi atapelekwa kwenye kituo cha kutolea huduma za afya kwa ajili ya kupatiwa matibabu n aushauri.

4.2.6 Wasafirishaji watakaokuwa hawana maambukizi wataruhusiwa kuendelea na safari baada ya kupewa cheti maalum ambacho kitadumu kwa siku 14.

4.2.7 Gari litakalokuwa na dereva ambaye amekutwa na maambukizi litafanyiwa utakasaji na timu ya maafisa afya wa mpakani kwa kuoshwa kwa maji na sabuni na kutumia *Alcohol based disinfectant* yenye kiwango cha asilimia 70 kabla ya kuruhusu dereva mwingine kuendesha gari hilo.

4.2.8 Gharama za utakasaji wa gari zitatozwa kwa mujibu wa Mwongozo wa Uchangiaji wa Huduma za Afya Mipakani wa Mwaka 2010.

## 4.3 Upimaji kwa wanaoingia nchini (Entry Screening)

4.3.1 Wasafirishaji wote wanaoingia nchini isipokuwa Watanzania hawataruhusiwa kuingia nchini bila kuonesha vyeti halali vya upimaji wa COVID-19.

4.3.2 Wasafirishaji ambao hawatakuwa na vyeti halali vya upimaji wa COVID-19 hawataruhusiwa kuingia nchini.

4.3.3 Wasafirishaji wote raia wa Tanzania waliopimwa nje ya nchi na kuonekana kuwa na **maambukizi** hata kama hawana dalili zozote hawataruhusiwa kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji hadi pale watakaporudiwa vipimo tena ili kujiridhisha kuwa hawana maambukizi.

4.3.4 Wamiliki wa magari wahakikishe wasafirishaji wao wote waliopima **na kuonekana kuwa na maambukizi** katika nchi jirani wanarudia vipimo kabla ya kuruhusiwa kuendelea na safari na wanatolewa taarifa kwa ajili ya ufuatiliaji na kupata huduma muhimu zinazostahili kutoka katika mamlaka za afya.

Mwongozo huu utaboreshwa kulingana na mahitaji

Prof. Abel N. Makubi.

**MGANGA MKUU WA SERIKALI**

Kiambatisho Na. 1

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF HEALTH, COMMUNITY DEVELOPMENT, GENDER, ELDERLY AND CHILDREN**


Telegram**"AFYA" DODOMA**
Telephone: **+25526-2323267**
Email: **ps@afya.go.tz**
(Allletersshould be addressed to
ThePermanentSecretary)

Government City – Mtumba,
Health Road/Street,
P.O.Box 743,
**40478 DODOMA.**


In replypleasequote:

**Ref. No. PA. 87/266/10. Vol.I/68** *(Date)_____/_______/2020*

***PoE-TD_COV:***

**TO WHOM IT MAY CONCERN**

## REF. CERTIFICATE OF HEALTH CLEARANCE

Please refer to the above heading.

I hereby certify that Mr/Ms ______________________________ has been tested for COVID-19 and found to be **NEGATIVE** on *(Date)*______________________.Therefore, the afore-mentioned person is allowed to proceed with his/her daily duties. The validity of this certificate is 14 days after testing.

Thank you for your compliance.

______________________

**Dr. Alex S. Magesa**
**Assistant Director for**
**Diagnostic Services**

______________________

**Prof. Abel N. Makubi**
**Chief Medical Officer**